



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO



Unapojibu tafadhali toja:

Kumb. Na: L.30/MMC-103/12

Tarehe: 23/02/2022

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA  
ZA ANWANI YA MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Morogoro, anapenda kuwatangazia nafasi 432 za Ajira ya muda kwa siku kumi (10), kwa nafasi za Wakusanya taarifa kwenye zoczi la Anwani za Makazi katika Kata na Mitaa yote ya Manispaa ya Morogoro.

**A: SIFA ZA WAOMBAJI:**

- (i) Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 – 40.
- (ii) Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- (iii) Awe anamiliki simu janja Android 4 na zaidi yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima (simu za Iphone hazikubaliki)
- (iv) Awe na barua pepe (email address) na nywila (password) inayofanya kazi.
- (v) Mwenye uwezo wa kusoma ramani atapewa kipaumbele.
- (vi) Awe ni mkazi wa Kata husika.
- (vii) Watumishi wote wa Idara ya Afya na Idara ya Elimu

**HAWARUHUSIWI KUOMBA.**

**B: KAZI NA MAJUKUMU:**

- (i) Kukusanya taarifa za Nyumba, Viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa Anwani za Makazi.
- (ii) Kuandika namba za Nyumba, Viwanja na maeneo ya huduma.
- (iii) Kutuma Data kwenye mfumo wa Anwani za makazi.
- (iv) Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku kumi (10).

**C: MAOMBI YAAMBATANISHWE NA:**

- (i) Nakala ya Cheti cha kidato cha Nne na kuendelea.
- (ii) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- (iii) Picha 2 (passport size).
- (iv) Barua ya maombi ipitie kwa Afisa Mtendaji wa Kata unayoishi.

**D: JINSI YA KUTUMA MAOMBI:**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu, barua pepe. Barua ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa Morogoro kwa mkono na siyo kwa Posta kwa anwani ifuatayo:-


**MKURUGENZI WA HALMASHAURI,  
MANISPAA YA MOROGORO,  
S.L.P 166,  
MOROGORO**

**E: MALIPO:**

Malipo ya kazi ni Tshs. 30,000.00 kwa siku.

**F: TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI:**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25/02/2022 saa 9:30 alasiri.

  
Ally H. Machelo  
**MKURUGENZI WA MANISPAA  
MOROGORO**

MKURUGENZI WA MANISPAA  
MOROGORO

Halmashauri ya Manispaa Morogoro, S.L.P 166 Morogoro, Simu/Nukushi Na: +255 023 2935242,  
Tovuti: [www.morogoro.go.tz](http://www.morogoro.go.tz), Barua Pepe: [info@morogoromc.go.tz](mailto:info@morogoromc.go.tz)